**MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA SITA**

**KISWAHILI I**

**MUONGOZO WA USAHIHISHAJI**

Mtahiniwa atoe majibu kama ifuatavyo:-

1. (a) **ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI**
   (b) Asili ya wabantu ni watu wanoishi kusini mwa jangwa la sahara
   (c)Kutafuta uhusiano uliopobaini ya lugha kadhaa za kibantu zilizoko eneo lote la wabantu katoka Afrika magharibi hadi Afrika mashariki
   (d) Lugha ni kipengele muhimu sana cha utamaduni kwa sababu kutumika kutambulisha jamii Fulani
   (e) Nchi ya Pwani

2. Aoneshe tofauti kati ya mofimu na viambishi kwa kuzingatia
   - Maana
   - Aina
   - Utendaji – Mofimu huru ni maneno kuruha yahitaji kupachikwa kwenye mizizi ya maneno ili kubainish adhana Fulani lakini viambishi vyote ni lazima vipachikwe katika vitenzi (mzizi) ili kubaini dhana Fulani.
   - Viambishi vinaweza kuwa mofimu ingawaje si kila mofimu yaweza kuwa kiambishi.

   Mfano (i)A –na-chez-a

   Ana na ni mofimu na pia ni viambishi.

   (ii) Mama ni mofimu lakini si viambishi

   **10hoja @ 02.5**

3. Mwanafunzi atoe maana ya umahiri wa lugha **(alama 1½)**
   Zifuatazo ni athari za mfumo wa elimu Tanzania katika umahiri wa lugha:
   - Mfumo kuruhusu Kiswahili kuwasomo na sisi kama lugha ya kufundishia
   - Mfumo kuruhusu kiingereza kufundishia masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili.
   - Mfumo kuruhusu baadhi ya shule hasa (binafsi) kutumia kiingereza kama lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi 1-7.
   - Mfumo kutojali /kutothamini maandiko ya Kiswahili (vitabu) na kuendeleza maandiko ya lugha nyingine (kiingereza katika elimu mfano vitabu hasa vya sayansi.
   - Mfumo kutothamini mchango na umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili na hivyo kusisitiza matumizi ya lugha ya kiingereza hasa mashuleni na wakati wote wa mawasiliano

     **5 hoja @ 1½**
     **Utangulizi 01**
     **Hitimisho 01**
     **Jumla 10**

4. Mwanafunzi aeleze dhima na maana ya maumbo kama ifuatavyo:

(i) 1- Kiambishi awali cha mtenda

2-Kiambishi awali cha mtendwa

3-Mzizi

(ii) 4- Kionyeshi

5-Kiambishi awali cha wakati uliopita

(iii) 6-kionyeshi

7-kiambishi awali kipatanishi cha kitu

8- kiambishi awali cha hali ya kuendelea

9-kiambishi awali rejeshi cha kitenda

**10- Mzizi**

**10 hoja @01**

5. Mwanafunzi atoe maana ya Sekta ya biashara
Ifuatayo ni namna sekta ya biashara ilivyotimiza azma ya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili
   - Kiswahili kimetumika katika kuandika nembo za vifungishio, pamoja na maelekezo ya matumizi ya bidhaa. Mfano; Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) inasisitiza kutoa maelezo yanayohusu bidhaa za dawa na chakula kwa Kiswahili.
   - Kutoa matangazo mbalimbali ya biashara katika mabango, vipeperushi, mitandaoni na kwenye vyombo vya habari kwa lugha ya Kiswahili.Mfano Azam TV imekuwa ikitoa matangazo mengi ya bidhaa za Azam na bidhaa za makampuni mengine.
   - Sekta ya biashara huratibu maonesho ya kimataifa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Mfano maonesho ya Sabasaba naNanenane.
   - Kupitia uwekezaji, sekta ya biashara huruhusu wawekezaji kuja kuwekeza na hujifunza lugha ya Kiswahili nao wakirudi kwao hutumia lugha hiyo ya Kiswahili, Mfano wawekezaji kutoka China, India Marekani.
   - Kufanya mikutano na semina za kibiashara, Mfano , semina za ujasiriamali, mikutano ya kitaifa na kimataifa

**hoja @ 03**
**Utangulizi 2½**
**Hitimisho 2½**

6. Mwanafunzi atoe utangulizi

   Hoja

   - Kuacha kushirikisha wenyeji katika usanifishaji
   - Walitumia sarufi ya lugha ya kiingereza kueneza dhana za kiswhaili , hivyo kukifanya kuwa na mwelekeo wa kiingereza
   - Kuacha kutumia lahaja nyingine zote za kutumia lahaja moja waliochagua ambayo ni kiunguja.
   - Hapakuwa na mkazo katika matumizi ya Kiswahili ikilinganishwa na lugha ya kiingereza.
   - Baadhi ya lahaja kubwa na zenye historia Keny zilipuuzwa na kuibua chuki na uhasama dhidi ya lahaja ya Pwani ya Zanzibar na mwambao wa bahari ya hindi.
   - Walikikikengeusha Kiswahili kwa kukipa matamshi ya kiingereza na hivyo kuharibu ladha yenye mvuto ya utamkaji wa lugha ya Kiswahili chenye asili ya kibantu.

     **5 hoja @03**

     **Utangulizi 02 ½**

     **Hitimisho 02½**

7. Mtahiniwa aandike barua kwa mhariri akizingatia muundo ufuatao

   i. Kichwa cha barua 03
   ii. Mwanzo wa barua 02
   iii. Kiini cha barua kuhusu athari za kutokufanya maandalizi na ushauri 07
   iv. Mwisho wa barua 01
   v. Jina la mwandishi 01
   vi. Anuani ya mwandishi 02
   vii. Tarehe 01

   Aidha mtahiniwa azingatie

   ✓ Matumizi ya lugha fasaha na sanifu 01
   ✓ Alama za uandishi 01
   ✓ Mpangilio mzuri wa barua 01

   **Jumla alama 20**

8. (a) Kigezo cha dhima kuu ya lugha.

   (b)Kigezo cha mada

   (c) Kigezo cha matumzi ya istilahi

(a) Kigezo cha dhima

- Dhima elezi – Hutumika kuelezea hisia za mwandishi
- Dhima arifu – Hutumika kutoa taarifa kuhusu jambo Fulani.
- Dhima amili – Huchochea hisia za msikilizaji au msomaji

(b) Kigezo cha mada

- Matini za kifasihi – Ni matini zinazohusu matini za kifasihi kama vile riwaya, tamthiliya na ushauri
- Matini za kisiasa- Ni matini za kimamlaka kama vile matini za kisiasa na kiserikali (hotuba na risala)
- Matini za kisayansi – Hujumuisha maswala yote ya kisayansi na teknolojia kwa mfano fizikia na kemia

(c) Kigezo cha matumizi ya istilahi.

- Matini ya kiufundi- Huwa na idadi kubwa ya istilahi.
- Matini za kunusu ufundi- Idadi ndogo au chache za istilahi
- Matini zisizo za kiufundi – Matini hizi ni zile ambazo hazina kabisa istilahi bali hutumia maneno ya kawaida kabisa.

**12 hoja @1½**

**Utangulizi 01**

**Hitimisho 01**